# SGR yazidi kunoga

Na Rehema Lugono, Kigoma

RAIS Samia Suluhu Hassan leo anatarajiwa kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kipande cha kutoka Tabora hadi Kigoma chenye urefu wa kilometa 506.

Waziri wa Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa alisema uwekezaji unaofanywa katika reli ya kisasa utaiwezesha Tanzania kuendelea kuwa lango muhimu la biashara kwa nchi za ukanda wa maziwa makuu na Afrika ya kati.

Profesa Mbarawa aliwaeleza waandishi wa habari Kigoma jana kuwa reli hiyo itaunganisha Kigoma na mikoa ya Tabora, Shinyanga, Mwanza, Dodoma, Morogoro na Dar es Salaam.

Alisema reli hiyo itarahisisha usafirishaji wa mizigo kutoka Bandari ya Dar es Salaam kwenda Kigoma na baadaye katika nchi jirani kupitia ushoroba wa kati.

Profesa Mbarawa alisema pia reli hiyo inayojengwa kwa Dola za Marekani bilioni 2.74 (Sh trilioni 7.2) itapunguza muda wa safari kati ya Dar es Salaam na Kigoma kutoka zaidi ya saa 30 zinazotumika sasa kwa reli ya kawaida hadi saa nane.

Alisema mradi huo pia utaimarisha mtandao wa reli kuelekea Musongati nchini Burundi kupitia kipande cha saba kutoka Uvinza hivyo kuongeza biashara ya kikanda na kuimarisha muunganiko wa uchumi kati ya Tanzania na nchi jirani.

Kwa mujibu wa Profesa Mbarawa, Mkoa wa Kigoma una nafasi ya kipekee kutokana na kuunganishwa na Ziwa Tanganyika linalowezesha huduma za usafiri na biashara kati ya Tanzania na nchi jirani zikiwemo Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Burundi na Zambia.

### Meli nne za mizigo

Wakati huo huo Rais Samia leo anatarajiwa kuzindua meli nne mpya za mizigo na kila moja ina uwezo wa kubeba tani 2,000 za mizigo.

Profesa Mbarawa alisema meli hizo zimejengwa na kampuni ya Gold Voyage Logistics ya China.

Alisema meli hizo zitaimarisha uwezo wa kusafirisha mizigo moja kwa moja kupitia Ziwa Tanganyika kwenda nchi jirani hatua inayolenga kukidhi ongezeko la biashara katika ukanda huo.

Profesa Mbarawa alisema takwimu zinaonesha katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 bandari za Ziwa Tanganyika zilihudumia tani 815,285 za shehena, ikilinganishwa na tani 397,897 zilizohudumiwa katika Mwaka wa Fedha 2024/2025.

"Meli hizi mpya zinaongeza nguvu ya ushirikiano kati ya serikali na sekta binafsi katika utoaji wa huduma za usafirishaji wa mizigo na zitachangia kuongeza ufanisi wa huduma kwa wafanyabiashara wanaotumia Ziwa Tanganyika," alisema.

Profesa Mbarawa alisema uzinduzi wa meli hizo ni sehemu ya jitihada za serikali za kuimarisha sekta ya uchukuzi na kutumia fursa za kijiografia ambazo mkoa wa Kigoma unazo kutokana na kuunganisha Tanzania na DRC, Burundi na Zambia kupitia Ziwa Tanganyika.

Alisema Rais Samia pia atakagua uboreshaji wa bandari ya Kigoma ambako linajengwa gati jipya la abiria na kuboresha gati la mizigo ili kuongeza uwezo wa bandari kuhudumia ongezeko la shehena na kuboresha huduma za usafiri wa majini.

"Miradi hiyo ya kimkakati inatekelezwa na serikali ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 inayolenga kujenga mfumo wa usafiri funganishi utakaounganisha reli, bandari na njia nyingine za usafiri ili kuongeza ufanisi wa uchukuzi, biashara na ukuaji wa uchumi," alisema Profesa Mbarawa.

## Serikali yataka heshima, weledi huduma kwa wastaafu

Na Mwandishi Maalumu

SERIKALI imeagiza Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali na watumishi wa Hazina Ndogo wawahudumie wastaafu kwa heshima, utu na weledi.

Waziri wa Fedha, Balozi Khamis Mussa Omar alitoa agizo hilo wakati akizungumza na watumishi wa Ofisi ya Hazina Ndogo Mkoa wa Tanga juzi.

Balozi Omar alisema wastaafu ni kundi linalostahili kuthaminiwa kutokana na mchango walioutoa katika ujenzi wa Taifa wakati wakiwa watumishi wa umma.

Alisema huduma bora kwa wastaafu huongeza ustawi wao na kuimarisha imani ya wananchi kwa serikali na akahimiza watumishi wawahudumie kwa uvumilivu, kuwapa maelekezo sahihi

kujihadhari na matapeli wanaojifanya mawakala wa huduma za pensheni.

Alisema huduma za pensheni na taratibu za uhakiki hazihitaji mstaafu kutoa fedha kwa mtu binafsi.

Kwa upande wake, Mhasibu Mkuu wa Serikali, Leonard Mkude na Msimamizi wa Ofisi za Hazina Ndogo nchini alisema Hazina ndogo ni sehemu muhimu ya mfumo wa serikali katika usimamizi wa fedha za umma nchini.

Mkude alisema ofisi hizo zimeanzishwa mahsusi kusogeza huduma karibu na taasisi za serikali zinazotekeleza bajeti katika ngazi za mikoa na hivyo kuongeza ufanisi, uwajibikaji, uwazi na nidhamu ya fedha katika utekelezaji wa majukumu ya serikali.



Alisema kwa sasa, Ofisi za Hazina Ndogo

Nipashe MWANGA WA JAMII
Jumatatu Julai 20, 2026

UZINDUZI

# Rais Samia kuzindua mradi wa trilioni 6/- SGR Kigoma

**Mwandishi Wetu**
0715086344 WhatsAPP SMS

RAIS Samia Suluhu Hassan leo anatarajiwa kuzindua na kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR), kipande cha sita (Lot 6) kutoka Tabora hadi Kigoma.

Mradi huo utakaotekelezwa kwa miezi 48 hadi mwaka 2030, ni miongoni mwa miradi mikubwa ya kimkakati itakayobadilisha uchumi wa ukanda wa Magharibi mwa Tanzania na nchi za Maziwa Makuu.

Kipande hicho cha sita, kina urefu wa kilometa 506, ujenzi wake utagharimu Sh6.31 trilioni na utatekelezwa na Kampuni ya China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC) chini ya usimamizi wa Shirika la Reli Tanzania (TRC).

Akizungumza na waandishi wa habari Julai 17, mwaka huu, Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, IGP Mstaafu Simon Sirro, alisema mradi huo utarahisisha usafirishaji wa mizigo na abiria, kupunguza gharama za usafiri na kuchochea biashara, uwekezaji na utalii.

"Mradi huu utawezesha usafirishaji wa haraka, salama na wenye gharama nafuu wa mizigo na abiria. Pia utafungua fursa mpya za biashara, uwekezaji na utalii kwa Mkoa wa Kigoma na nchi jirani," alisema Sirro.

Kwa mujibu wa mkataba, ujenzi huo utakamilika ndani ya miezi 48 na unatarajiwa kutoa ajira zaidi ya 15,000 kwa wakazi wa Tabora na Kigoma.

Aidha, safari kutoka Dar es Salaam hadi Kigoma zinatarajiwa kupungua hadi takribani saa saba hadi nane, tofauti na zaidi ya saa 20 zinazotumika kwa usafiri wa barabara.

Mradi huo pia, unatarajiwa kuunganisha Bandari ya Dar es Salaam na masoko ya Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), huku muda wa usafirishaji wa mizigo kuelekea DRC ukipungua kutoka takribani siku 30 kwa malori hadi saa 36 kupitia reli.

Akizungumzia mradi huo, Mchambuzi wa Uchumi, Dk Emmanuel Kiwia, alisema mradi wa Tabora-Kigoma una umuhimu mkubwa kwa sababu unaibadilisha Kigoma kutoka kuwa mwisho wa reli kuwa kitovu cha biashara za kikanda.

"Miundombinu ya reli ina uwezo wa kubadilisha kabisa mwelekeo wa uchumi wa eneo husika. Kigoma sasa inaweza kuwa lango la biashara kati ya Tanzania, DRC na Burundi kwa kiwango kikubwa zaidi kuliko ilivyowahi kushuhudiwa," alisema.

Alisema gharama za usafirishaji ni miongoni mwa vikwazo vikubwa vya ushindani wa biashara katika Afrika Mashariki, hivyo ujio wa reli hiyo utaongeza ufanisi wa mnyororo wa usambazaji wa bidhaa.

"Kupungua kwa gharama za usafirishaji kunamaanisha bidhaa za Tanzania zitafika sokoni kwa bei nafuu zaidi. Hii itaongeza ushindani wa wafanyabiashara na kuvutia wawekezaji wanaotafuta maeneo yenye miundombinu imara," alisema.

Dk Kiwia, alieleza manufaa ya mradi huo hayatabaki kwenye sekta ya usafiri pekee, bali yataenea kwenye kilimo, viwanda, biashara na huduma mbalimbali zinazozalisha ajira.

"Historia inaonyesha kila reli kubwa duniani imezalisha miji mipya ya biashara. Tunaweza kuona ukuaji wa vituo vya uzalishaji, maghala na viwanda vinavyotegemea usafirishaji wa haraka wa mizigo," alisema.

Mchambuzi mwingine wa uchumi, Dk Eligius Kibamba, alisema mradi huo ni uwekezaji wa muda mrefu unaolenga kuimarisha nafasi ya Tanzania katika biashara ya kikanda na kimataifa.

"Leo tunaangalia reli kama njia ya usafiri, lakini kiuchumi tunapaswa kuiona kama nyenzo ya kuongeza ushindani wa taifa. Nchi yenye miundombinu bora huvutia mitaji na biashara kwa kasi zaidi," alisema.

Alisema Kigoma ina nafasi ya pekee kutokana na ukaribu wake na DRC, ambayo ni moja ya masoko makubwa zaidi barani Afrika yenye mahitaji makubwa ya bidhaa na huduma.

"DRC ina watu zaidi ya milioni 100. Kuunganisha soko hilo na Bandari ya Dar es Salaam kupitia reli ya kisasa ni fursa ambayo inaweza kuongeza mapato ya biashara kwa kiwango kikubwa sana," alisema.

Dk Kibamba, alisema reli hiyo pia itapunguza uchakavu wa barabara unaosababishwa na malori ya mizigo, jambo litakalopunguza gharama za matengenezo ya miundombinu ya barabara kwa Serikali.

"Faida nyingine ambayo mara nyingi haisemwi ni kupungua kwa gharama za matengenezo ya barabara. Mizigo mingi ikihamia reli, Serikali itaokoa fedha ambazo zinaweza kuelekezwa kwenye huduma nyingine za maendeleo," alisema.

Aliongeza kuwa mafanikio ya mradi huo yatategemea pia uwekezaji katika maeneo ya viwanda, maghala ya kisasa na huduma za usafirishaji zitakazoongeza matumizi ya reli mara baada ya kukamilika kwake.



Rais Samia Suluhu Hassan

WORLD BANK GROUP